# TOA HOFU JUU YA AFYA YAKO

### Ushauri Nasaha na Upimaji ni nini?

Ni mazungumzo kati ya mshauriwa ambapo mshauri atakusikiliza, atajibu maswali yako, atakusaidia kuyatazama upya maisha yako, kama vile wapi kuna uwezekano kuwa ulijihatarisha kupata uambukizi ya UKIMWI. Pia mshauri nasaha atakusaidia kupanga mkakati mpya ili kuzuia uwezekano wa kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI katika siku zijazo. Haya yote yanafanywa kitaalamu.

### Faida za ushauri nasaha na upimaji

- Ukijua hali yako itakusaidia kuondoa mashaka na wasiwasi
- Kama hujaambukizwa virusi, utachukua tahadari zaidi ili usiambukizwe. Pia itakufanya kubadili tabia
- Kama utakuwa umeambukizwa virusi vya UKIMWI
  - Utawezeshwa kutambua namna ya kuishi bila ya kupata maambukizi zaidi
  - Utaelewa jinsi ya kuishi bila ya kuambukiza wengine
  - Utashauriwa mambo ya kuzingatia ili uishi kwa muda mrefu
  - Utaelekezwa kwenye huduma za dawa za kupungua makali ya virusi vya UKIMWI na huduma nyingine muhimu, lishe bora na kuwahi kutibu magonjwa nyemelezi

### Faida kwa Mwanamke anayetarajia kubeba mimba

- Kama utakuwa umeambukizwa virusi vya UKIMWI, utafahamishwa athari za kubeba mimba ukiwa umeambukizwa
- Pia kama una mimba tayari, utaelekezwa jinsi ya kupata huduma ili kuzuia maambukizo kwa mtoto

### Nitarajie nini niemdapo kupima virusi vya UKIMWI

Unapokwenda kupima una haki ya kupata huduma bora ambayo in pamoja na

- Ushauri Nasaha kabla na baada ya kupimwa
- Ushauri inatolewa mahali pa faragha
- Upimaji ulio wa siri (Majibu hayatolewi kwa mtu mwingine bali wewe peke yako)

### Walengwa ni akina nani?

- Ni watu wote
- Vijana wake kwa waume wanaotaka kujua hali zao ili waweze kuwa na uhakika na maisha yao
- Vijana wanaopanga uchumba au wanaotarajia kufunga ndoa
- Wanandoa au wengine wanaopanga kupata mtoto
- Wanafamilia

Na iwapo utaamua kupima damu ili ujue hali yako, utapata majibu yako siku ile ile baada ya muda mfupi.

*Karibuni sana!*

# Upo Gizani Kuhusu Afya Yako?



Vipeperushi hivi viliandikwa na
Dafrosa Mbuya, Mshauri Nasaha,
na kufadhiliwa na Geneva Global, USA

**St Luke's Dispensary**
SLP 2, Mpwapwa, Tanzania
Tel: 026 232 0652, E-mail: stlukes@tarlings.com